JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Simu Nambari**: 255-26-2360033**

E-MailNo**. bustanitc@gmail.com**

Mobile No. 0758 900881
0756 876122
0752 36330
0743133331

Chuo cha Ualimu Bustani,
S.L.P. 131,
KONDOA.

16/05/2022

NDG:…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA ASTASHAHADA YA ELIMU MSINGI NA AWALI KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023

1.0 UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukuarifu rasmi kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Astashahada ya Ualimu katika Chuo Cha Ualimu Bustani. Chuo kina dhamira ya kuwa kituo cha kuibua na kuendeleza stadi za Ualimu kwa kujikita katika maeneo ya Sayansi na Technolojia, Sayansi ya Jamii, Sayansi Asilia (Natural Science), masomo ya Ualimu,ujasiliamali na stadi za maisha ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji nchini. Hivyo unapaswa kuthamini uchaguzi huu kwa kusoma kwa bidii, kufuata taratibu na kanuni za Chuo ili uweze kufikia malengo yako binafsi na malengo ya Taifa kwa ujumla.

2.0 MAHALI CHUO KILIPO

Chuo cha Ualimu **Bustani** kipo Mkoa wa **Dodoma,** Wilaya ya **Kondoa**. Kipo kilometa mbili kutoka kondoa mjini (stendi kuu ya mabasi)

3.0 TAREHE YA KURIPOTI CHUONI

Unatakiwa kuripoti Chuoni tarehe 13/06/2022 bila kukosa. Iwapo hutafika Chuoni baada ya tarehe 30/06/2022 hutapokelewa. Mara baada ya kuwasili Chuoni fika ofisi ya usajili ambapo utapokelewa na kupewa maelekezo.

Wakati wa usajili unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo:

i) Fomu ya maelekezo ya kujiunga na Chuo (Joining instruction)

ii) Cheti halisi cha kumaliza kidato cha nne (**School Leaving Certificate**- Original) na Cheti halisi cha kufuzu kidato cha nne (**Academic Certificate of Secondary Education, O-Level**) au **Result Slip** kama vyeti havijatoka na hasa wale waliomaliza kidato cha nne mwaka 2021, na nakala zake.

iii) Cheti halisi cha kuzaliwa-(**birth certificate**) na nakala yake.

iv) **Cheti cha daktari/medical examination form**, ikiwa imejazwa na daktari wa Hospitali ya Serikali ya Wilaya au Mkoa.

4.0 VIFAA

4.1 Mashuka mawili rangi ya blue bahari, blanketi 1, mto 1, chandarua nyeupe 1 na foronya 2 za blue bahari zisizofumwa

4.2 Vyombo vya kulia chakula (sahani 1, kikombe 1, bakuli 1, kijiko 1) galoni ya lita tano ya plastiki Kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa yaliyochemshwa, pamoja na ndoo moja ya lita kumi kwa ajili ya kuoge

4.3 VIFAA VYA MICHEZO

4.3.1 Bukta na T-shirt rangi yoyote pamoja na raba jozi moja ya rangi yoyote, track suti rangi ya blue bahari kwa ajili ya mchakamchaka na jogging siku za Jumamosi na ziara za kimichezo.

4.4.0.**VIFAA VYA TAALUMA.**

4.4.1 Daftari zisizopungua 20 QUIRE 3 , kalamu za wino na risasi, mkebe wa Hisabati.

4.4.2 Mkoba wa kazi utapatikana chuoni

4.4.3.unatakiwa kuja na muhtasari wa masomo yote ya shule za msingi na awali.

4.4.4. Karatasi **rimu 1 (A4**) rangi nyeupe yenye karatasi 500 kwa muhula.

5.0 ADA YA CHUO

Ada ya mafunzo ni **Tsh 450,000/=** kwa mwaka, kwa muhula unatakiwa kulipa kiasi kisichopungua **Tsh 225,000/=** Fedha hiyo unapaswa kuingiza kwenye simu ya mtandao wowote na utapata maelekezo ya namna ya kulipa ada kwa kutumia **control** number ukifika Chuoni. Mwanachuo hatasajiliwa ikiwa atakosa ada.

6.0. MICHANGO YA CHUO

Mbali na fedha hiyo utatakiwa kutoa michango katika maeneo yafuatayo

.

6.1 Ulinzi 30,000/= kwa mwaka.
6.2 Ukarabati 25,000/= kwa mwaka.
6.3 Usafi na mazingira 20,000 kwa mwaka.
6.4 Huduma ya kwanza 10,000/= kwa mwaka.
6.5 Michezo 30,000/= kwa mwaka.
6.6 Kukodi Godoro 10,000/= kwa mwaka.
6.7 Usajili na kitambulisho 20,000/= kwa mwaka.
6.8 Mchango wa serikali ya wanachuo 5000/= kwa mwaka.
6.9 Mchango wa bima ya afya (NHIF) 50,400/= **kwa asiyekuwa nayo**

Jumla ya michango ya Chuo Tsh **195,400**/= kwa mwaka ziwekwe kwenye account namba **50201100020 (NMB) (BUSTANI TEACHERS' COLLEGE FUND**) bila kukosa (Mwanachuo hatasajiliwa akikosa michango)

Mchango wa serikali ya wanachuo **5,000/=** iwekwe kwenye account namba **50210010117 (NMB) (BUSTANI STUDENT ORGANISATION).**

N.B Wasilisha risiti za malipo ya bank kwa msajili ukifika Chuoni. Aidha usije na fedha tasilimu chuoni. **usichanganye** akaunti kwani fedha ikilipwa kimakosa hairudishwi.

7.0 SARE ZA CHUO



WANAUME

i. Suruali mbili nyeusi za kushonwa.
ii. Mashati mawili ya blue bahari yenye mikono mirefu.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye visigino vifupi.
iv. Soksi nyeupe jozi mbili.
v. Sweta jeusi na koti linalofanana na suruali.
vi. Tai nyeusi.
vii. T- shirt ya chuo – uje na Tshs 20,000/=

NB: Ili kupata mfanano wa sare za chuo na zinazokubalika unashauriwa kupata maelekezo ya kina kutoka chuoni kabla hujashona



WANAWAKE;

i. Sketi mbili nyeusi mshono wenye rinda katikati, ndefu inayokaribia na kisigino kama inavyoonekana katika mchoro.kwa waislamu “umbrella” inayofanana na shati.
ii. Mashati mawili ya blue bahari yenye mikono mirefu.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye visigino vifupi.
iv. Soksi nyeupe jozi mbili
v. Sweta jeusi na koti linalofanana na sketi.
vi. Tai nyeusi
vii. T- shirt ya chuo – uje na Tshs 20,000/=

NB: Ilikupata mfanano wa sare za chuo na zinazokubalika unashauriwa kupata maelekezo ya kina kutoka chuoni kabla ya kushona au kununua.

8.0 MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA YA WANACHUO

i. Mwanachuo anashauriwa aje na fedha tasilimu kwa ajili ya matumizi binafsi.
ii. Mwanachuo mwenye kadi ya bima ya afya anatakiwa kuja nayo.
iii. Mwanachuo asiye na kadi ya bima ya afya atatakiwa kujiunga na mpango wa bima ya afya ya Taifa (NHIF). Hivyo kila mwanachuo asiye na Bima aje na kiasi cha Tsh. 50,400/= kwa ajili ya kupata Bima ya afya kwa mwaka mzima.
iv. Mwanachuo atapaswa kufanya uchunguzi wa afya katika Hospitali za wilaya au mikoa kwa kutumia fomu iliyoambatanishwa hapo chini.
v. Kila mwanachuo atatakiwa kuchangia gharama ya mahafali kwa kadri ya makubaliano yatakayofanywa na Uongozi wa serikali ya wanachuo kwa kiasi kisichopungua Tshs10,000/=

9.0 CHAKULA

Chuo hutoa chakula kwa wanachuo wote
Chuo hakitoi chakula maalum (special diet)

10.0 SHUGHULI ZA UZALISHAJI MALI CHUONI

Ili kutekeleza mtaala wa mafunzo ya **E l i m u y a Ualimu** kwa ufanisi Chuo kinaendesha shughuli za kilimo hususani mazao ya bustani na ufugaji. Lengo kuu ni kuwafanya wanachuo wajifunze kwa nadharia na vitendo katika masomo yao hususani stadi za kazi, ili kutekeleza mtaala wa **Ualimu ambao unazingatia falsafa ya elimu ya kujitegemea unatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo; jembe-wote, Reki – wavulana tu, Fagio ndefu za chelewa – wasichana tu.** Ili kuendeleza utoaji wa huduma katika maeneo hayo kutakuwa na utaratibu wa kuchaguliwa wanachuo kwa zamu angalau mara moja kwa kipindi chote cha mafunzo kubaki chuoni wakati wa likizo kwa lengo la kuendeleza utoaji wa huduma katika bustani, mifugo na mazingira ya chuo kwa ujumla.

11.0 MWISHO

Jumuiya ya chuo cha Ualimu Bustani inakutakia maandalizi mema ya safari ya kuja chuoni.
KARIBU SANA

JOYNA ELISHA CHANAFI
MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
BUSTANI CHUO CHA UALIMU
KONDOA!

NAKALA:

(a) :Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S L P 10,
DODOMA.

(b) Mkurugenzi Mafunzo ya Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S L P 10`,
DODOMA.

(c) Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule (K)
Kanda ya Kati,
DODOMA

(d) Afisa Elimu (M),
DODOMA

(e) Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo,
DODOMA

SHERIA NA KANUNI

Pamoja na maelekezo yaliyotolewa hapo juu zifuatazo ni sheria na kanuni za chuo ambazo utatakiwa kuzifuata wakati wote wa mafunzo, kama utaona ni ngumu kuzifuata usije kwa sababu ndizo zinazowezesha kila mwanachuo kufikia malengo yake binafsi,ya chuoni na Taifa kwa ujumla.

Sheria na kanuni zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII, TABIA NJEMA na HAIBA NA MAADILI YA MWALIMU kwa ujumla. Sheria hizi zinahusu:-

1. MIGOMO

Marufuku kwa mwanachuo kuhamasisha, kuanzisha, kuchochea au kushiriki migomo ya aina yoyote chuoni, mwanachuo anapaswa kufuata taratibu katika kutatua matatizo yake au ya wanachuo wenzake wakati wote wa mafunzo.

ADHABU: ***ATAKAYE BAINIKA NA MAKOSA HAYA ATAACHISHWA MAFUNZO MARA MOJA***

2. MAVAZI BORA NA YA HESHIMA

Kila mwanachuo anatakiwa avae mavazi ya heshima yanayolingana na haiba na kazi ya Ualimu.

I. ***Mavazi hayo yanatakiwa yawe***;

a. Yasiyobana mwili
b. Yasiyoonesha maungo vya mwili

II. Hairuhusiwi kwa mwanachuo;

a. kutoka nje ya chuo bila ya sare za chuo (unatakiwa kuvaa sare za chuo pindi unapokuwa nje ya chuo)
b. Kunyoa kipara au mtindo wowote au kufuga kucha
c. Kufuga ndevu
d. kuvaa vitu kama vile mapambo mfano Heleni,Mikufu, Bangili n.k
e. Kuvaa mlegezo au nguo za mtindo, mfano - model
f. T-shirt zenye maandishi au zisizo na staha
g. Wasichana kuvaa suruali, Sketi au magauni mafupi (sketi au magauni yanatakiwa yavuke magoti kwenda chini)
h. Wasichana kusuka mitindo au rasta

III. Inaruhusiwa kwa wanachuo

a. Wasichana kubana nywele nyuma kama ni ndefu
b. Wasichana wasiosuka au kubana wanatakiwa kuwa na nywele fupi zisizokuwa na mtindo wowote
c. Wasichana kusuka nywele za twende kilioni (utii wa roda) au kunyoa kawaida
d. Wavulana kuwa na nywele fupi zisizo kuwa na mtindo wowote

N.B: kipengele cha mavazi kuhusu suruali kitafafanuliwa kulingana na mazingira husika kama vile prepo,kulala, michezoni, nk

ADHABU: ***ATAKAYE KIUKA HAYA ADHABU KALI ZA KINIDHAMU ZITATOLEWA IKIWA NI PAMOJA NA KUACHISHWA MAFUNZO***

3. NIDHAMU

Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu kwa kuwaheshimu watu wote ndani na nje ya chuo

I. Kila mwanachuo lazima asalimiane na wenzake, aamkie walezi wake pamoja na watu wote
II. Kila mwanachuo anatakiwa kutii na kutekeleza kanuni zilizowekwa, kama vile
    a. Kutii kengele inapopigwa
    b. Kutii bendera ya taifa
    c. Kuitika majina(roll-call) mahali na muda husika
    d. Kuwahi mahali anapoitwa iwe ukumbini,darasani,bwaloni n.k

e. Kuwahi wito anapoitwa na walezi au viongozi wa serikali ya wanachuo
f. Kukimbia mchakamchaka
g. Kuvaa kitambulisho
h. Kuhudhuria paredi Jumatatu, Jumatano na Ijumaa
i. Kuhudhuria vipindi vyote darasani bila kukosa

III. Kujituma katika kazi zote, ndani na nje ya darasa kwa muda wote atakao kuwapo chuoni
IV. Kutii na kufuata maelekezo halali yanayotolewa na viongozi wa serikali ya wanachuo
V. Kuheshimu serikali ya wanachuo kama vile Raisi, Mawaziri, Viongozi wa madarasa na Mabweni

ADAHABU: ***ATAKAYEKIUKA ADHABU KALI ITATOLEWA IKIWA NI PAMOJA NA KUACHISHWA MAFUNZO***

4. UHUSIANO WA KIMAPENZI

I. Hairuhusiwi kuwa na mahusiano ya kimapenzi wakati wowote wa mafunzo yako, wanachuo kwa wanachuo au wanachuo na mtu mwingine yeyote
II. Kuolewa au kuoa wakati wa mafunzo ni marufuku
III. Hairuhusiwi kubebesha/kubeba au kutoa mimba
IV. Hairuhusiwi kujiingiza katika tabia ya uasherati na umalaya, kama vile
    a. Kujiuza (uchangudoa)
    b. Kupiga picha za utupu au Kutuma picha za utupu
    c. Usagaji
    d. Ushoga
    e. Na mengine yanayofanana na hayo hasa matumizi mabaya ya simu na mitandao
V. Hairuhusiwi wanachuo wawili wa jinsi tofauti kukaa faragha yani peke yao hasa nyakati za usiku

ADHABU: ***UKIKIUKA MOJA KATI YA HAYA UTAACHISHWA MAFUNZO MARA MOJA***

5. ULEVI

Ni marufuku kwa mwanachuo kutumia kilevi chochote kile ndani na nje ya chuo kipindi chote cha mafunzo. Vilevi hivyo ni kama:-

I. Pombe aina yoyote ile
II. Dawa za kulevya aina yoyote
III. Uvutaji wa Sigara
IV. Ulaji wa mihadarati. Mf Mirungi,Bangi, Tambuu n.k
V. Hairuhusiwi kuingia kwenye majumba ya starehe mf. Baa , Disko n.k
VI. Hairuhusiwi kuingia kwenye vilabu vya pombe
VII. Hairuhusiwi kuingia kwenye nyumba za kulala wageni

ADHABU: ***UKIPATIKANA NA KOSA MOJAWAPO KATI YA HAYA UTAACHISHWA MAFUNZO MARA MOJA***

6. NYUMBA ZA WAKUFUNZI /WAFANYAKAZI

Mwanachuo hairuhusiwi kwenda kwenye nyumba za wakufunzi au wafanyakazi bila ya kibali cha **Ofisi ya Uadili** au mkuu wa chuo

ADHABU: ***ATAKAYEKIUKA ADHABU KALI ITATOLEWA***

7. KUWAHI

I. Mwanachuo anatakiwa kufika chuoni kwa tarehe iliyopangwa ya kufungua chuo au kama amepewa ruhusa
II. Mwanachuo anatakiwa kwenda kwa mlezi/mzazi pindi tu chuo kitapofungwa au kuruhusiwa si vinginevyo

ADHABU: ***ATAKAYEKIUKA ADHABU KALI ITATOLEWA IKIWEMO KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA MAFUNZO***

8. <u>KAZI ZA MIKONO NA USAFI</u>

Kila mwanachuo anatakiwa kushiriki kikamilifu katika kazi , kama vile

I. Kazi za mikono kama vile uzalishaji mali (E.K)
II. Usafi wa mazingira ya chuo kama vile:
    a. Mabwenini
    b. Madarasani
    c. Mazingira yote kwa ujumla. Mf vyooni,bafuni na sehemu nyingine
III. Usafi binafsi

ADHABU: ***ATAKAYEKIUKA ADHABU KALI ITATOLEWA***

9. <u>UTUNZAJI MALI</u>

I. Kila mwanachuo anatakiwa atunze mali za umma (chuo) kama vile
    a. Viti
    b. Meza
    c. Madawati na
    d. vifaa vingine mbalimbali kama vile
        majembe
        reki
        mifagio
        soketi
        mashoka nk
II. Kila mwanachuo anatakiwa atunze mali zake binafsi na za wenzake
III. Ni kosa Kupoteza, au kusababisha mali zako kuibiwa kwa uzembe
IV. Marufuku kuondoka na kifaa chochote mahali popote bila ya idhini ya mamlaka husika

ADHABU: ***ADHABU KALI ITATTOLEWA KWA ATAKAYE HARIBU AU KUPOTEZA PAMOJA NA KULIPA KIFAA HUSIKA***

10. <u>UTORO</u>

I. Kila mwanachuo anatakiwa awepo mahali anapohitajika kwa muda uliopangwa kama vile
    a. Darasani
    b. Bwenini
    c. Uwanjani
    d. Sehemu za usafi wa mazingira ya chuo.
II. Awepo na ashiriki katika shughuli za uzalishaji mali kwa muda husika/tajwa

ADHABU: ***ADHABU KALI ITATOLEWA KWA ATAKAYEKIUKA***

11. <u>LUGHA</u>

Ni marufuku kwa mwanachuo kutumia lugha ya

I. Matusi
II. Kuudhi, kukebei, dhihaka au kusengenya
III. Lugha za mitaani (kihuni)
IV. Hairuhusiwi kuwa mbishi unapoelekezwa jambo jema
V. Hairuhusiwi kuwa muongo
VI. Hairuhusiwi kuwa mgomvi
VII. Haruhusiwi kugombana
VIII. Hairuhusiwi kuwapiga wafanyakazi au wakufunzi au wanachuo wenzako

ADHABU: ***ENDAPO UKIKIUKA MOJA KATI YA HAYA ADHABU YAKE KUSIMAMISHWA MAFUNZO MARA MOJA AU ADHABU KALI ZA KINIDHAMU ZITATOLEWA***

12. <u>WIZI</u>

Ni marufuku kwa mwanachuo kuwa mwizi au mdokozi wa mali za chuo au wafanyakazi/wakufunzi, za wanachuo wengine au za mtu mwingine yeyote

ADHABU: ***ATAKAYEBAINIKA KUTENDA KOSA HILI ATAACHISHWA MAFUNZO MARA MOJA***

13. <u>RUHUSA</u>

I. Ruhusa zote za kulala nje ya chuo zitatolewa na ***<u>mkuu wa chuo</u>***

II. Ruhusa ya kutoka nje ya chuo ndani ya siku zitatolewa na mkufunzi wa zamu au mwadili wa wanachuo baada ya masomo au siku za jumamosi au jumapili

III. Ni marufuku kuhama bweni pindi unapopangiwa (unaweza kuhama pindi unapopata kibali toka **Ofisi ya Uadili**)

IV. Wakati wa kufika(kuripoti) chuoni,ni marufuku kwa mwanachuo kuingia na kukaa bwenini; mpaka awe amepata kibali toka ***Ofisi ya Uadili*** kupitia ***ofisi ya usajili***

V. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote chuoni pasipo na kibali cha ***mkuu wa chuo*** na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kinatakiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa ***mkuu wa chuo***

VI. Hairuhusiwi kufanya siasa ndani ya chuo, katika kipindi chote uwapo chuoni

VII. Hairuhusiwi kwa mwanachuo kijipika chakula chuoni.

ADHABU***: YEYOTE ATAKAYETENDA MAKOSA HAYA; PASIPO KUWA NA KIBALI CHA MKUU WA CHUO, MWADILI AU MKUFUNZI MTEULE ATAPEWA ADHABU KALI,PAMOJA NA KUACHISHWA MAFUNZO MARA MOJA***

14. <u>MATIBABU</u>

I. Mwanachuo atatibiwa katika zahanati ya chuo kwanza

II. Mwanachuo ataenda hospitali kwa ruhusa ya Daktari/Nesi/Mratibu wa afya wa Wanachuo

III. Mwanachuo mwenye matatizo ya kiafya lazima awe na kibali cha daktari halali wa hospitali ya serikali ili kupangiwa kazi kulingana na afya yake

ADHABU: ***ATAKAYE TENDA KOSA KATI YA MAKOSA HAYA ATAPEWA ADHABU KALI YA ONYO***

15. <u>KUTEMBELEWA NA WAGENI CHUONI</u>

I. Mwanachuo haruhusiwi kutembelewa na wageni siku ya Jumatatu hadi Ijumaa

II. Mwanachuo haruhusiwi kuonana na mgeni wake mpaka awe amepata kibali cha mwadili au Mkufunzi wa zamu

III. Mizigo yote anayoletewa mwanachuo inatakiwa ifike ***<u>Ofisi ya Uadili</u>*** kwanza

IV. Mwanachuo haruhusiwi kumsindikiza mgeni nje ya chuo bila ya kibali cha **Ofisi ya Uadili** au **Mkufunzi wa Zamu**

V. Mwanachuo haruhusiwi kumlaza mgeni wake bwenini

ADHABU: ***ATAKAYEKIUKA ATAPEWA ADHABU KALI***

16. <u>MICHANGO</u>

I. Wanachuo wote wanatakiwa kulipa michango yote kama walivyoagizwa katika fomu ya kujiunga na chuo

II. Michango yote inayoagizwa na chuo ni mali ya serikali hivyo matumizi yake huzingatia kanuni za fedha za serikali

ADHABU: ***KUTOTIMIZA NI KUKIUKA KANUNI ZA CHUO NA UNATAKIWA KURUDI KUFUATA MICHANGO HUSIKA***

17. <u>MATUMIZI YA SIMU ZA MKONONI</u>

I. Simu za mkononi haziruhusiwi kuwashwa wakati wa masomo iwe darasani au wakati wa kujisomea mwenyewe(prep)

II. Simu za mkononi haziruhusiwi kupigisha mziki madarasini au mabwenini au maeneo yoyote ya chuo

III. Simu za mkononi haziruhusiwi kutuma picha zisizo na maadili au jumbe zisizokuwa na maadili kwa wengine au mitandaoni
IV. Unapaswa kulinda simu yako au kifaa chochote cha thamani kama laptop: ni kosa kusababisha upotevu au usumbufu wowote

ADHABU: ***ATAKAYEBAINIKA ATANYANG'ANYWA SIMU MPAKA MWISHO WA MAFUNZO YAKE AU ADHABU KALI ITATOLEWA AU VYOTE KWA PAMOJA***

18. <u>VIFAA VYA UMEME</u>

Hairuhusiwi kuwa na vifaa vya umeme kama pasi,heater,redio, birika la umeme, n.k

ADHABU: ***ATAKAYE KUTWA NA VIFAA HIVI ATANYANG'ANYWA NA ADABU KALI ITATOLEWA***

19. <u>MAFUNZO KWA VITENDO (MUV)</u>

I. Ruhusa zote za kutoka nje ya kituo zitatolewa na ***<u>mkuu wa chuo kushirikiana na mwalimu mkuu wa shule uliopangiwa</u>***
II. Ruhusa ya kutoka kituo kimoja kwenda kutembea kituo kingine zitatolewa na **mwalimu mkuu wa kituo**
III. Ni marufuku kuhama kituo ulichopangiwa (unaweza kuhama pindi unapopata kibali toka **ofisi ya taaluma** kwa sababu maalum)
IV. Wakati wa kufika(kuripoti) kituoni,ni marufuku kwa mwanachuo kujitenga au kukaa peke yake ; mpaka uwe umepata kibali toka ***Ofisi ya chuo*** kwa sababu maalum.
V. Ni marufuku kwa mwanchuo kutumia lugha ya Matusi,Kuudhi, kukebei,dhiaka kusengenya au Lugha za mitaani (kihuni)
VI. Hairuhusiwi kuwa mbishi unapoelekezwa jambo jema
VII. Hairuhusiwi kuwa muongo, mgovi au kugombana
VIII. Hairuhusiwi kufanya mapenzi wakati wowote wa mafunzo yako; kati ya wanachuo kwa wanachuo, wanachuo na mtu mwingine yeyote au mwanachuo na mwanafunzi
IX. Kuolewa au kuoa wakati wa mafunzo ni marufuku
X. Hairuhusiwi Kujiuza (uchangudoa),Kupiga picha za utupu au Kutuma picha za utupu, Usagaji, Ushoga na mengine yanayofanana na hayo

ADHABU: ***ENDAPO UKIKIUKA MOJA KATI YA HAYA ADHABU YAKE KUSIMAMISHWA MAFUNZO MARA MOJA AU ADHABU KALI ZA KINIDHAMU ZITATOLEWA***

ZINGATIO

Unataarifiwa kuwa chuo hiki ni cha Serikali wala siyo cha DINI. Hivyo kinazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu, kila mwanachuo huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao. Pia kuwa na vipindi vya dini katika ratiba za masomo.

Wanachuo hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba ya chuo au baada ya vipindi tofauti na ratiba iliyowekwa

KUWA MWALIMU BORA NA MWENYE MAADILI INAWEZEKANA , TIMIZA WAJIBU WAKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Simu Nambari**: 255-26-2360033**
E-MailNo**. bustanitc@gmail.com**
Mobile No. 0758900881
0756 876122
075236330
0743133331

Chuo cha Ualimu Bustani,
S.L.P. 131,
KONDOA.

16/05/2022

Mimi ……
Niliye chaguliwa kujiunga na CHUO CHA UALIMU BUSTANI mwaka 2022/2023 nimesoma maelekezo ya kujiunga na chuo pamoja na sheria na taratibu za Chuo hivyo ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yangu binafsi, Malengo ya Chuo na Taifa kwa ujumla .

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu na nyeti kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika mafunzo yangu nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajila yangu pia. Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa , nikiwa chuoni:

1. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu kama Mwalimu tarajali
2. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za chuo kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazo tolewa mara kwa mara na uongozi wa Chuo
3. Sitajihusiha na vitendo vya utovu wa nidhamu katika muda wote wa mafunzo
4. Nitakubali kupewa huduma stahiki kama chakula kulingana na taratibu na uwezo wa Chuo
5. Nitashiriki katika shughuli zote za nje ya darasa kwa moyo wa kizalendo ili kukitumikia chuo na taifa langu.
6. Ikiwa nitakikiuka kiapo hiki pamoja na kanuni na taratibu za chuo kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/mlezi wangu……(Jina la Mzazi/Mlezi) kwa ajili ya hatua zaidi na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayotolewa na Kamati ya nidhamu ya Chuo kwa mujibu wa sharia na taratibu za chuo.

Saini ya Mwanafunzi……Tarehe……
……

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi……..
ninakubali kupokea nafasi yakijana wangu (jina)……..kujiunga katika Chuo cha Ualimu Bustani mwaka 2022. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya chuo kwa wakati kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na chuo. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na Chuo kwa kulipa michango kwa wakati ili kumwezesha mwanangu kutekeleza wajibu wake kwa chuo na Taifa kwa ujumla .

Anuani yangu ya kudumu, S.L.P……...
Wilaya ……..
Mkoa …….
Makazi…….
Shughuli/kazi……

Simu…….
Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nitajulisha Chuo kwa maandishi ili kurahisisha mawasiliano

Saini ya mzazi/mlezi……Tarehe ……

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Principal
Bustani Teachers' College,
P.O.BOX 131,
KONDOA

TO: The Medical Officer

…….

PART A:

Please examine Mr/Mrs/Miss……..
To his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.

B: Blood Group

Date : …….. Signature……

Official Stamp

PART B: MEDICAL CERTIFICATE.

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time teacher Education course.

I. (a) Eye – sight……
(b) Hearing……...
(c) Limbs……
(d) Speech…….
(e) Leprosy…….

II. Neuroses……

III. Other serious diseases……..

IV. Pregnancy……

Date:…….. Signature……

Official stamp